# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**FRIENDS SCHOOL KAMUSINGA HIGH**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

**FRIENDS SCHOOL KAMUSINGA KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016**

**102/3**

**Karatasi 3**

**Mwongozo wa kusahihisha**

1. a) Haya ni maneno ya Diwani III akizungumza na siki wakiwa nyumbani kwa Diwani III. Hii ni baada ya mgomo wa kufanya kazi kufanyika mjini. 4 x 1

b)

- Wazalendo – wanapigana na uongozi mbaya wa cheneo
- Ni wanamapinduzi – wanajaribu kuleta uongozi mpya.
- Ni wenye ari katika kazi yao – siki hafuti kazi yake.
- Ni wenye kuaminika – siki anamwanini Diwani III anapozungumza.
- Ni wenye utu – siki alijitahidi katika zahanati ya cheneo.Zozote 4 x 2

c) Balagha
methali
(Mwanafunzi atoe mifano) zozote 2 x 2

d) Migomo ya wafanyakazi
ukosefu wa dawa
mishahara mjini
ukosefu wa mlo wenye lishe. (4 x 1 )

**SEHEMU B: RIWAYA**

2. Haya ni maneno ya mtemi Nasaba Bora kwa nduguye Majisifu wakiwa kwa mtemi Nasaba Bora. Huu ni wakati alipotembelewa na mwalimu majisifu kwake. zozote 4 x 1

b) (i) Hakupenda watoto wake walemavu
(ii) Hakufunza kama alivyotakikana katika shule ya upili ya Nasaba Bora.
(iii) Alikuwa mlevi na mpyaro
(iv) Aliwibia mswaada wa kidagaa kimemwozea
(v) Hakuelewana na nduguye zozote 4 x 2

c) Mswaada wa Amani uliibwa na mwalimu majisifu.
- Unyakuzi wa ardhi ya Chichiri Hamadi na mwinyi Hatibu mtembezi na mtemi Nasaba Bora.
-Kuchoma makao ya mamake imani
-Kufunga Amani na Imani kizuizini bila hatia yote.
-Kuwekelea Yusufu makosa na kumuweka kizuizi.
-Kuweka kitoto nje ya kibanda cha Amani.
-Kupiga Amani kwa kufikiria ana uhusiano na Zuhura na kumwacha akiwa amezirai.
- Kutombeba Amani alipokuwa akitoka siku ya wazalendo. Zozote 4 x 2

3. Madhubuti anachagua kujitafutia kazi yake badala ya ile babake alimtafutia.
-Imani alikunywa maji ya mto kiberenge na kuvunja mwiko uliokuwepo.
-Amani na Imani walikaa chumba kimoja bila kufanya uzinifu wowote.

-Amani aligawa shamba lao kwa watu wengi.
-Imani alilea watoto walemavu wa Dora.
-Amani na Imani walilea kitoto walichopata badala ya kukitupa kama alivyofanya mtemi Nasaba Bora.
-Amani hakulipiza kisasi baada ya mtemi Nasaba Bora kumpiga na kumtupa
-Amani na madhubuti walitafuta ushahidi uliofanya Yusufu achiliwe.
-Amani alikataa kuchukua uongozi baada ya mtemi Nasaba Bora kuondoka.
-DJ aliwasaidia Amani na Imani kupata kazi sokomoko walipoenda. Zozote 10 x 2

4. (i) Muungano
(ii) Tathlitha
Ukara
(iii) Lina mishororo mitatu kila ubeti
Lina ukwapi na utao
Vina vya kati vinabadilika na mwisho havibadiliki
Mizani kumi na sita kila mshororo
Halina kibwagizo.
(iv) Tuweke nyoyo zetu zikiwa nzuri bila kulalamika
Tutakayo yanyooke bila ugomvi
Yale tunayotenda yatuletee mafanikio
(v) Inkisari – Choyo, hakie
Mazida – tuelekezane
Tabdila – machukiyo hunuko
Kuboronga sarufi – ilete mema mavuno
(vi) Usonono – kuhuzunisha
Msagurano – kuzozana

1. Ulumbi – uhodari wa kuzungumza au kuiga mazungumzo kwa usaniina uhodari mkubwa.
Soga – Ni utanzu mdogo wa fasihi simulizi unaotumiwa kwa ajili ya kuchekesha, kukejeli au kuumba au kufanya dhihaka ili kupitisha wakati.
b)

- Hukejeli matendo Fulani ya binadamu kama vile uovu.
- Huburudisha wasikilizaji
- Huelimisha jamii
- Huelekeza wanajamii
- Huonyesha utani ulioko baina ya wanajamii zozote 4 x 2

c)

- Huwa na ujuzi wa kina wa utamaduni husika
- huwa na tajriba ndefu ya maisha

- Huwa na ufundi wa kutumia tamathali za usemi
- Huvalia malemba ili kuvutia hadhira
- Anastahili kuwa na sauti inayosikika bila matatizo yoyote.
- Anastahili kuwa mwenye ushawishi mkali.
- Ana uwezo wa kushirikisha hadhira yake
- Anatumia miondoko na ishara
- Ana uwezo wa kughani mfululizo. Zozote 8 x 1

6. Maghani ni utungo wa kishairi ambao hutongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji, yaani kalimia. (al 2)

B. (i) Tondozi – Ni utungo wa kutukuza watu, wanyama au vitu vingine.

(ii) Sifa – Ni utungo unaosimulia kwa undani matukio ya kishujaa yanayohusiana na mtu anayesifiwa kuanzia mwanzo wa mapambano hadi ushindi unapopatikana.

(iii) Tendi – Ni usimulizi mrefu wa kishairi unaotungwa papo kwa papo na huelezea tukio kuu la kihistoria kwenye jamii.

(iv) Rara – Utungo wa kishairi wenye ubunifu mkumbwa unaokusudia kusisimua na unatongolewa kwa kuibwa au kughanwa ukiambatanishwa na ala za muziki.

c) Ni tungo za kishairi

-Husimulia matukio kwa kirefu
-Hutungwa papo hapo na kusemwa mbele ya hadhira
-Huwa na majisifu
-Hutolewa na mtu mmoja au kundi la watu.
-Huwa na uigizaji
-Hutumia tamathali za usemi zozote 3 x 2

d)

-Kuliwaza
-kuhamasisha
-Kutia moyo
-Kusifu
-Kukashifu
-Kujigamba
-Kuburudisha zozote 4 x 1

7. a) Haya ni maneno ya rafikiye mwakitawa akimwambia mwakitawa kuhusu mama mmoja ambaye amekuwa akiangalia nyumba yao kwa kutumia darubini. (4 x 1 )

b)

- Uuzaji wa binadamu k.m kananda anauziwa dereva wa kongo
- Uzinifu kati ya mwatela na kananda.

- Wizi wa watoto k.m mwakitawa aliibiwa kutoka kwa mamake na Mwatela.
- Ukatili k.m kananda aligongwa kwa jiwe na Mwakitawa. Zozote 4 x 1

c)

- Mwakitawa alishikwa na woga mwingi
- Babake mwakitawa alifikiria kulipa majambazi wamwangamize kananda
- Mwakitawa alipiga mamaye kananda kwa jiwe na kumumiza
- Babake Mwakitawa alihuzunika sana baada ya kusikia kananda amepigwa,.
- Kulitokea ugomvi baina ya Mwatela na mkewe na akataka mwakitawa kuelezwa kweli kuhusu mamake.
- Kananda alilazwa ili apate matibabu.
- Mwatela pia alilazwa na kupata matibabu.
- Mwatela alitafuta wakili na kumrithisha mali yake kananda.
- Mwakitawa na mamake kananda walikutana na kuungana naye zozote 8 x 1 = 8